



# KUTANA NA CARMEN

## kutoka Lebanoni

*Kutana na watoto wa Msingi wakiwasaidia wengine, kama Yesu alivyofanya.*



Yote kuhusu Carmen



**UMRI:**  
miaka 8

**KUTOKA:**  
Syria lakini sasa anaishi Lebanoni

**LUGHA:**  
Kiarabu, Kingereza

**MALENGO NA NDOTO:**

- 1) Kutembelea hekalu.
- 2) Kuwa msanii.
- 3) Kutumikia misheni.



**FAMILIA:**  
Carmen anao dada wawili wakubwa na kaka mmoja mkubwa.

VIELEZO NASVETLA RADYOVEVA

## Mikono Saidizi ya Carmen

Carmen na mama yake wanaishi huko Lebanoni, lakini walikuwa wakiishi huko Syria. Majirani zao wanatokea Syria pia. Desemba iliyopita, Carmen alitaka kufanya kitu cha ukarimu kwa ajili yao. Kila siku hadi Krismasi, Carmen alinunua kitu kimoja kidogo kutoka dukani. Aliviweka vyote kwenye boksi. Baada ya siku 25, boksi lilikuwa limejaa. Siku ya Krismasi, Carmen alilichukua lile boksi na kulipeleka kwa majirani zake. Walishukuru sana. Carmen anasema huduma yake ilimsaidia yeye kukumbuka huduma ambayo Yesu Kristo aliitoa. "Tunapoonyesha upendo kwa wengine," Carmen anasema, "sisi tunauhisi upendo wa Mungu." ●



**Carmen anamfuata Yesu kwa kuwasaidia majirani zake. Geuza ukurasa ili kusoma hadithi kuhusu jinsi Yesu alivyotufundisha kuwapenda majirani zetu.**

Mambo Pendwa ya Carmen




**HADITHI KUHUSU YESU:**  
Wakati Yesu alipotembea juu ya maji



**MAHALI:**  
Ufukweni



**CHAKULA:**  
Tambi, aiskrimu ya matunda



**WIMBO WA MSINGI:**  
"My Heavenly Father Loves Me"  
(Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 228-29)

**SOMO SHULENI:**  
Sayansi



**RANGI:**  
Zambarau isiyokolea

**Jiunge na Timu ya Mikono ya Usaidizi!**



Unapowahudumia wengine, wewe unakuwa sehemu ya Timu ya Mikono ya Usaidizi! Je, unaweza kumhudumia nani?